

02.04.2026

**TANGAZO LA ZABUNI YA KUTENGENEZA VIFAA VYA ZIMAMOTO KCU (1990) LTD**  
**MSIMU 2026/2027**

Zabuni na: KCU/CN/2026/2027/03

1. Kagera Cooperative Union imetenga fedha kwa ajili ya kuingia makubaliano ya kimkataba na mtoa huduma ya utengenezaji vifaa vya zimamoto kwa msimu 2026/2027.
2. Mwombaji aambatishe nakala kibali kutoka kwenye mamlaka husika chenye kuruhusu utengenezaji wa vifaa vya zimamoto kwa muda unao ombewa kazi.
3. Mwombaji aambatishe nakala zinaoonesha vielelezo vya kazi alizowahi kufanya.
4. Mwombaji aambatishe nakala ya wasifu wa kampuni.
5. Kampuni/shirika liambatishe nakala ya kusajiliwa na BRELA.
6. Kampuni/shirika liambatishe nakala ya leseni pamoja na TIN.
7. Ombi la zabuni liwe na jina na anwani halisi ya mwombaji, aidha aoneshe mahali Ofisi ilipo. (Physical address)
8. Mwombaji ataje gharama za kufanya sevisi ya vifaa vipya vya zimamoto.
9. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 100,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955002 General A/C**
10. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo namba 2-7 vilivotajwa hapo juu.
11. Bahasha ya maombi ifungwe vizuri katika Lakiri na kuandikwa juu yake:- **"MAOMBI YA ZABUNI YA YA KUTENGENEZA VIFAA VYA ZIMAMOTO MSIMU 2026/2027"** kwa anwani tajwa hapa chini,

MENEJA MKUU,  
KCU (1990) LTD,  
P.O BOX 5,  
BUKOBA.

12. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika Ofisi ya Manunuzi KCU kabla au mnamo tarehe 20.04.2026 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumatatu na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika sherehe ya ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni.
13. Maombi yatakayochelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.

Imetolewa na;

MENEJA MKUU

